

Katika Manispaa za Kinondoni na Ubungo ni kata tatu ndizo zilizoainishwa katika mpango huu ambazo ni Tandale, Mburahati na Mwananyamala. Katika maeneo hayo kutakuwa na miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja na vivuko, njia za waenda kwa miguu (Foot paths), taa za barabarani (Street lights), vizimba vya taka ngumu (Solid waste collection centres) na vituo vya mabasi.

3) UJENZI WA MTO SINZA (mto Ng'ombe).

Katika Manispaa ya Kinondoni, mradi huu utatekelezwa kwa ujenzi wa mto Sinza (Mto Ng'ombe) wenye urefu zipatazo km.7.5 ili kupunguza mafuriko yanayotokana na kujaa kwa mto huo wakati wa mvua. Mto huo unapita katika kata za Ubungo, Sinza na Manzese katika Manispaa ya Ubungo na Kijitonyama, Tandale, Mwananyamala, Magomeni, Makumbusho na Ndugumbi zilizopo katika Manispaa ya Kinondoni.

4) MIRADI MINGINE

Mradi wa DMDP unahusisha pia maeneo mengine k.m uimarishaji na uboreshaji wa mfumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo ya kielektroniki na mfumo wa taarifa za kijiografia, Kujenga uwezo wa watalaam katika fani mbalimbali kwa kutoa mafunzo na vifaa na uendeshaji wa Halmashauri; uimarishaji wa mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayatokelezwa katika Halmashauri; kujenga uelewa na elimu juu ya uendeshaji wa miradi ya ubia kati ya Serikali kuu na sekta binafsi wa uboreshaji wa mfumo unganishi kati ya sekta ya usafirishaji na mipango ya matumizi ya ardhi.

3.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI NA MALIPO YA FIDIA.

Utekelezaji wa miradi iliyoanishwa hapo juu unafanyika kwa awamu kulingana na mpango wa manunuzi (Procurement Plan) uliokubaliwa kati ya Benki ya Dunia na Serikali kupitia Ofisi ya Rais –Tamisemi na Halmashauri.

Katika Mwaka wa fedha 206/2017 miradi iliyoanza kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa barabara tano kati ya kumi na moja zilizoanishwa kama miradi ya awamu ya kwanza. Barabara hizo ni Makumbusho- Sokoni, MMK,Nzasa,TanESCO -Soko la Samaki, na Viwandani. Ujenzi wa barabara hizo unaendelea. Aidha zabuni kwa ajili ya barabara sita (Zinazohitaji fidia) zilishatangazwa na taratibu za tenda zipo katika hatua ya mwisho.

4.0 MALIPO YA FIDIA

Hivi karibuni Serikali imeridhia maombi ya Halmashauri ya kuzipatia fedha kugharamia malipo ya fidia katika maeneo yote yanayohitaji kulipiwa fidia. Tayari uhakiki katika baadhi ya maeneo hayo umekamilika na malipo yameandaliwa. Serikali imeshatoa idhini ya malipo kwa barabara za Makanya, Tandale- Kisiwani, Kilongawima na Simu 2000. Na katika awamu ya kwanza jumla wa wafidiwa 179 watalipwa fidia zao baada ya kukamilisha taratibu za kahasibu pamoja na kuwasilisha nyaraka zao ikiwa pamoja na akaunti zao za Benki.

Halmashauri inasubiri idhini ya malipo katika barabara za Kilungule na Kilimani ili malipo yaweze kukamilika katika barabara zote.